

Kuongezea kutokana na mihimili midogo

- Unapopanda mihimili midogo, panda umbali wa sentimita 5 hadi 10 na kina cha sentimita 5.
- Funika kwa karatasi ya plastiki ili kuharakisha uotaji na kuhifadhi unyevu na kiwango cha joto.
- Kama matawi ni mengi kutoka kwa mhimili yaondoe baadhi yake.
- Kata na upande katika shamba baada ya kifikia sentimita 30.
- Mihimili yenye afya kwa mazao ya juu.



Mihimili yenye mazao mengi



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Mutura I. M

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Embu

S.L.P. 27 Embu

Simu: 068 20116/20873

Nukulishi: 068 30064

Baruapepe: kariembu @salpha .co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 33 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Ukuuzaji haraka wa viazi vitamu



Utangulizi

Viazi vitamu ni moja wapo wa vyakula vikuu vya nyumbani na vya kuuza nchini Kenya. Pato lake linasitishwa na uhaba wa asilia za kupandia. Hii ni kwa sababu ya kukauka kwa mihimili wakati wa kiangazi na sampuli zingine kuwa na mihili michahce mno. Teknolojia ya ukuzaji wa haraka wa mimea hii hufanikisha uzalishaji wa haraka na kihifadhi hasa wakati wa kiangazi. Mbinu hii aidha huzuia magonjwa na wadudu.

Kitalu cha viazi vitamu

Tayarisha kitalu cha kupandia viazi vitamu sawia na vile vya karoti au kabeji. Hii iwe ni mwezi mmjoja kabla ya wakati wa kupanda au asilia za kupanda zinapohitajika. Kama mchanga huna rutuba ya kutosha ongezea mbolea ya samadi au ya dukani.

Kutayarisha asilia

Uchaguzi wa mmea

Mimea ya kupandwa iwe ni yenye nguvu au iliyo na afya na kuwa na sifa zinazohitajika.



Kuchagua mimea shambani

Kutayaisha miche ya kupanda

- Kata sentimita 30 za mche uliyochaguliwa na uwe vipande viwili kila kimoja na tawi.
- Zamisha kila kipande kwenye dawa ya kopa kwa muda wa dakika 30 ili kuzuia maambukizi ya magonjwa kisha uweke kwenye kitalu.



Ukataji wa miche midogo

Kupanda miche katika kitalu

- Chimba mashimo madogo ya upana wa penseli ili kupanda.
- Kama kitalu ni cha kuhifadhi mashimo yawe na umbali wa sentimita 5x3 au 1x1 kama itahamishwa baada ya mwezi mmoja.
- Panda miche ile na jicho moja likiwa mchangani.



Kupanda katika kitalu

- Funika kitalu kwa karatasi ya nailoni au kifunikio kingine na kisalie hapo hadi asilimia 80 ya uotaji ifanyike.



Kitalu chenye kivuli

- Ihamishe miche kutoka kwa kitalu hadi shambani baada ya mwezi mmoja wakati hali ya anga ni mwafaka.